**Jina……………………………………..Darasa……………………Nambari………….**

**Tarehe …………………………………..Sahihi……………………**

**2019**

**TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA**

**INSHA**

**KIDATO CHA TATU**

**MAAGIZO**

Insha yako isipungue maneno 300

Andika insha kuhusu jinsi ya kuhifadhi mazingira katika eneo gatuzi lenu. Alama 20

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Macho ya Abdul yalipigwa na mwali mkali wa jua la asubuhi. Ilikuwa ndiyo mara yake ya kwanza kuuona mwanga halisi wa ombwe lijiitalo dunia tangu alipohukumiwa kifungo gerezani. Punde tu komeo la mlango wa seli lilipofunguliwa, ilimlazimu Abdul ayafumbe macho kabla ya kuyafumbua tena taratibu ili yazoee mabadiliko yake.

Ilikuwa ndiyo siku ya Abdul ya kuachiliwa huru kutoka kwenye kifungo kirefu kilichoyapa macho yake mazoea ya giza la kaburi mle gerezeni. Macho yake yalipokwishaizoea ile hali na kumhakikishia kuwa kila alichokuwa akikiona si kizuka ila uhalisia, alipiga hatua. Akatoka nje ya mlango wa seli, kisha kwa kutoamini, akageuka nyuma kulitazama tena lile pango alimokuwa ametikwa katika muda huo wote. Akayafikicha macho kwa kutoamini huku machozi yakimdondoka asijue kama yalikuwa ya furaha au ya huzuni. Alipogeuka kuanza safari ya uhuru wake, macho yake yalikumbana na lango la gereza. Hapo, akasita kidogo, labda kuhakikisha kama kweli alikuwa huru. Bila shaka, hakuna askari wa gereza aliyemshikia bunduki au kumuamuru asimame. Walimtazama tu na kumpa tabasamu.

Taratibu, Abdul aliendelea kupiga hatua. Mhemko aliokuwa nao kutokana na hewa safi iliyompenya mapafuni uliufanya moyo wake upige kwa kasi. Ghafla, tabasamu ikapasua mashavuni pake. Akasita. Akaiinua pua yake iliyompa hakikisho kuwa uvundo na uozo wa seli haukuwa naye tena. Ingawa mwili wake ulijaa mabaka ya uchafu na matambara yaliyouficha uchi wake kuvunda, hilo halikumkera tena. Kwa hivyo, akatia tena tabasamu. Lake kuu lilikuwa shukrani kwa kuepuka yale madhila ya joto na rundo la wafungwa. Na kama hilo halikutosha, aligeuka tena ili sasa kuliangalia lile gereza. Bila kutarajia, alipiga magoti, akainua mikono kupiga dua, ―Ewe Mungu, niepushe na balaa nyingine.

Safari ya Abdul kutoka katika majengo ya gereza ilikumbwa na mseto wa mawazo. Alipokuwa katika ujia uliomwelekeza katika barabara kuu, mambo mengi yalimpitikia mawazoni asipate jawabu. Hakujua kama wazazi wake walikuwa wangali hai, na kama walikuwa bado wanaishi katika nyumba ile ya kukodi kwa miaka hiyo kumi aliyokuwa jela. ‗Je, nikiwakosa, nitaenda wapi? Nitaanzia wapi kuwatafuta?' Mawazo hayo yaliifungua mifereji ya machozi, kisha ile ya makamasi. Balagha hiyo ilimfikisha katika kituo cha magari ya uchukuzi kwa ule aliouona kuwa muda wa kufumba na kufumbua. Aliyafuta machozi yake haraka kwa kiganja kisha akaziba tundu la pua, tayari kupenga kamasi. Hata hivyo, kabla hajafanya hivyo, nafsi yake ilimtahadharisha kuwa hatua hiyo ingekatiza uhuru aliopewa kwa kuchafua mazingira. Kwa hivyo akaghairi. Akavuta ncha ya shati lake na kuitumia kama hankachifu kutimiza azma yake.

Hapo kituoni, matatu iliyokuwa mbele ilikuwa na watu wachache. Abdi akaingia na kukaa upande wa kioo ambapo tafakuri nyingi zilimjia. Akakumbuka jinsi kesi yake ilivyoendeshwa kinyume kabisa na ukweli na hukumu kutolewa kinyume cha haki. Mimi Abdul, mtoto twaa tangu kuzaliwa kwangu hata mdudu sijawahi kumponda kwa udole wangu, ndiyo sasa nije

kusingiziwa kuua mtu? Mungu wangu! Kwa nini dunia hii haina wema? Kwa nini wanaodaiwa kuwa wasomi hata wakapewa jukumu la kuwakilisha maslahi ya raia ndio wanaowadhulumu hao raia? Hivi, hata hukimu na tajiriba yake aliamua kufuatilia zile porojo za wanaojiita majasusi? Angeahirisha hukumu yake ili kufanya uchunguzi zaidi, bila shaka nisingepata mapigo na dhuluma hizo zote. Kwa kweli, hii ni dunia ya mwenye nguvu mpishe! Abdul alijisemea.

**Maswali**

(a) Kwa nini Abdul alifungwa? (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

(b) Kwa kurejelea kifungu eleza mashaka katika asasi za kurekebisha tabia. (alama 4)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

(c) Ni kinyume kipi kinachoonekana katika kifungu hiki? (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

(d) Ni mambo yapi yaliyomtia Abdul machugamachuga alipoachiliwa huru. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

(e) Abdul anaelekea kuwa na hulka gani? Fafanua kwa kurejelea kifungu. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

(f) Msamiati ufuatao una maana gani kwa mujibu wa kifungu hiki. (alama 2)

(i) Ombwe…………………………………………………………………………………………

(ii) Mhemko………………………………………………………………………………………

**MATUMIZI YA LUGHA** **ALAMA 35**

a) Eleza tofauti kati ya sauti hizi. Alama 4

i) /y/ na /z/

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

ii) /t/ na /h/

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

b) Andika katika ukubwa wingi. Alama 2

Ndovu amezaa ndama mkubwa sana.

…………………………………………………………………………………………

c) Toa mfano wa neno lenye silabi ya konsonanti pekee alama 1

…………………………………………………………………………………………

d) Akifisha alama 2

Tupa kifaa cha kunolea kisu na air conditioner huuzwa kwa bei ghali.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

e) Amrisha katika nafsi ya tatu wingi. Alama 2

Uandike insha ndefu.

…………………………………………………………………………………………..

f) Badilisha sentensi hii katika usemi wa taarifa. Alama 2

“Itakubidi urauke alfajiri iwapo unataka kusafiri nami kesho,” mjomba alisema.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

g) Andika vinyume vya vitenzi katika sentensi ifuatayo. Alama 2

Chebet aliingia garini na kufunga kioo.

…………………………………………………………………………………………

h) Viorodheshe vipashio vya lugha ukianza na cha juu Zaidi. Alama 2

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

i) Ainisha mofimu katika: alama 3

Alinywewa maziwa

j) Tambua wakati na hali katika sentensi ifuatayo. Alama 3

Mhazigi atakuwa ameiunganisha mifupa iliyovunjika

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

k) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi ‘tahini’. Alama 2

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

l) Neno hili limo katika ngeli gani? Alama 1

Kinda

……………………………………………………………………………………………

m) Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari. Alama 1

<u>Kundi la wachawi</u> lilitiwa mbaroni jana.

……………………………………………………………………………………………

n) Andika katika wingi alama 2

Mtoto wake alilelewa kwenye ukoo huu

……………………………………………………………………………………………

o) Yakinisha alama 2

Wakulima wasipopalilia mahindi yao hawatapata mazao.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

p) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari alama 4

Mwanahamisi alilishona rinda lake vizuri.

q) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo alama 3

Waliochezewa

**ISIMUJAMII** **ALAMA 10**

"…maandiko yanasema kwamba siku ya kiama tutapaa angani na mwenye uwezo."

a) Tambua sajili ya kauli iliyopo hapo juu. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

b) Kwa kutoa mifano mwafaka, taja sifa bainifu za sajili uliyoitambua hapo juu. (alama 8)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**FASIHI SIMULIZI** **ALAMA 20**

a) Eleza sifa zozote tano za hadithi (alama 10)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

b) Eleza sifa za mtambaji bora wa ngano (alama 10)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………